



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU TAASISI/ASASI ZILIZOPATA VIBALI VYA KUTOA
ELIMU YA MPIGA KURA KWENYE UCHAGUZI MDOGO WA UDIWANI
Dodoma, 30 Novemba, 2022**

Kifungu cha 4C cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 kinaipa mamlaka Tume ya Taifa ya Uchaguzi kutoa Elimu ya Mpiga Kura nchi nzima, kuratibu na kusimamia Taasisi/Asasi na watu wanaotaka kutoa Elimu hiyo.

Kwa ajili ya Uchaguzi Mdogo wa Udiwani kwenye kata 12 za Tanzania Bara, Tume ilizialika Taasisi/Asasi zinazotaka kutoa Elimu ya Mpiga Kura kupitia vyombo mbalimbali vya habari kati ya tarehe 30 Oktoba, 2022 na tarehe 9 Novemba, 2022 kutuma maombi. Jumla ya Asasi tatu zilituma maombi.

Baada ya uhakiki na upembuzi wa maombi yaliyopokelewa, Tume katika kikao chake cha tarehe 25 Novemba, 2022 iliridhia Taasisi/Asasi zifuatazo kupewa vibali kwa ajili ya kutoa Elimu ya Mpiga Kura: -

| NA. | JINA LA TAASISI/ASASI | ANUANI | ENEO LA KAZI |
|-----|--|----------------------|----------------------|
| 1. | Tanzania Building Future Organization (TABUFO) | S. L. P. 289 Mtwara | Kata ya Mnumbwe |
| 2. | Tanzania Peace, Legal Aid and Justice Centre (PLAJC) | S. L. P. 3497 Dodoma | Kata ya Dabalo |
| 3. | Umbrella of Women and Disabled Organization (UWODO) | S. L. P. 650 Njombe | Kata ya Njombe Mjini |

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inazikumbusha Taasisi/Asasi hizo kuwa zitawajibika kujigharamia katika zoezi la kutoa Elimu ya Mpiga Kura.

Nassoro B. Shemzigwa

KAIMU MKURUGENZI WA UCHAGUZI